

JARIDA LA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



Wizara ya Furaha

Toleo la Mtandaoni: 01 | 03 Agosti, 2022 - TABORA | www.habari.go.tz

UFUNGUZI WA MASHINDANO YA UMITASHUMTA 2022 WAPAMBA MOTO



Wizara_SanaaTz





**MASHINDANO YA
MICHEZO YA UMITASHUMTA 2022
YANAENDELEA MKOANI TABORA**

03 Agosti, 2022



Maandalizi Ufunguzi UMITASHUMTA Yamekamilika

Na Shamim Nyaki - TABORA

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbasi leo Agosti 3, 2022 amefanya mahojiano kupitia kipindi cha DARAJANI kinachosikika kupitia Radio Uyui FM 99.3 Tabora.

Kupitia kipindi hicho Dkt. Abbasi amesema maandalizi ya ufunguzi wa Mashindano ya UMITASHUMA mwaka 2022 mjini Tabora tayari yamekamilika na yanatarajiwa kufunguliwa rasmi hapo kesho Agosti 4, 2022 na Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa.

Aidha ametumia wasaa huo kuzungumzia mafanikio ya Serikali ya awamu ya sita katika sekta za sanaa, utamaduni na michezo.



Makatibu Wakuu Wakagua na Kuridhika na Maandalizi ya Ufunguzi UMITASHUMTA

Na Shamim Nyaki - **TABORA**

Makatibu Wakuu wa wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbasi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Prof. Riziki Shemdoe na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Francis Michael jioni ya Agosti 03, 2022 katika Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi Tabora wamekagua na kuridhika na maandalizi

ya ufunguzi wa Mashindano ya michezo kwa shule za Msingi (UMITASHUMTA).

Mashindano hayo yatazinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) , Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Agosti 04, 2022.

Viongozi mbalimbali wa

Mkoa, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Balozi Dkt. Batilda Buriani walikuepo katika ukaguzi huo.

Aidha, Wasanii Beka flavour na Meja Kunta wametoa burudani fupi uwanjani hapo.











Soka Wasichana Yafika Hatua ya Makundi UMITASHUMTA 2022

Na Shamim Nyaki - TABORA

Katika mashindano ya Shule za Msingi (UMITASHUMTA) yanayoendelea mkoani Tabora mwaka huu wa 2022, mchezo wa Soka kwa Wanawake ni mionganini mwao.

Kufikia Agosti 03, 2022 tayari mchezo huo umefika hatua ya Makundi ukiwa na idadi ya makundi manne, yenye ushindani wa hali ya juu.

Mkoa wa Manyara umezoa alama 12, na kuwa mbele ya Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Singida na Kagera, huku kundi B likiongozwa na Mkoa wa Mwanza wenye alama 12 mbele ya Mtwara, Tanga, Iringa na Ruvuma.

Katika Kundi C, Vijana kutoka Mkoa wa Mara tayari wamebeba alama 9 wakiongoza Mikoa ya Geita, Shin-

yanga, Kilimanjaro na Simiyu.

Vilevile, kundi D lenye Mikoa ya Lindi, Dodoma, Katavi na Arusha, Mkoa wa Tabora umefanikiwa kuwa na alama 12 hadi sasa.



Soka Wavulana Watinga Hatua ya Makundi UMITASHUMTA 2022

Na Shamim Nyaki - TABORA

Mashindano ya michezo kwa Shule za Msingi (UMITASHUMTA) kwa mwaka 2022 yanaendelea mkoani Tabora, huku Vijana wakionenesha vipaji na uwezo wa hali ya juu.

Katika michezo hiyo, Agosti 03, 2022 mchezo wa Soka tayari umeingia katika hatua ya Makundi kwa upande wa

wavulana ambapo kuna kundi a hadi c.

Katika kundi A, Mkoa wa Pemba unaongoza kundi hilo ukiwa na alama 9 mkononi ukiitangulia Mikoa ya Iringa, Singida, Katavi, Mara na Simiyu.

Kundi B mpaka sasa Geita imekaa kileleni ikiwa na

alama 8 ikiacha nyuma Mikoa ya Shinyanga, Njombe, Mtwara, Tanga, Rukwa na Kilimanjaro.

Aidha, kundi C linaongozwa na Mkoa wa Kagera kwa alama 10 ukiitangulia Mikoa ya Pwani, Tabora, Manyara, Arusha na Songwe.

**MASHINDANO YA MICHEZO KWA SHULE ZA
MSINGI (UMITASHUMTA) YANAENDELEA
MKOANI TABORA HUKU WANAFUNZI
WAKIENDELEA KUONESHA VIPAJI KATIKA
NYANJA MBALIMBALI.**





UMITASHUMTA | UMISSETA 2022



MKOA WA MARA
UMITASHUMTA 2022

MKOA WA MARA
UMITASHUMTA 2022

PENIBA
UMITASHUMTA



#SensaBika

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo



